BUNGE LA GATUZI LA TAITA TAVETA
OFISI YA SPIKA WA BUNGE
speaker@taitatavetaassembly.go.ke

IJUMAA, TAREHE 6 SEPTEMBA, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MGOMO WA WAHUDUMU WA AFYA

Bunge la Gatuzi la Taita Taveta linaendelea kusikitikia mgomo wa wuhudumu wa afya katika Kaunti ya Taita Taveta, ambao umeingia siku yake ya tatu leo hii. Hili ni kufuatia notisi ya mgomo, iliyotolewa na vyama kadhaa vya wahudumu hao wa afya, mnamo tarehe 21 Agosti, 2024.

Mgomo huu wa wahudumu wa afya umesababisha kukatizwa kwa huduma muhimu za afya katika kanti hii. Ni suala la luhuzunisha kuwa mamia ya wananchi wa Kaunti hii wanaotafuta matibabu katika hospitali zetu wanakosa huduma hizo, huku huduma za dharura pia zikiendelea kusitishwa, na hili limepelekea kuhatarishwa kwa Maisha ya wananchi wa Taita Taveta wanaotafuta huduma za afya katika hospitali zetu.

Bunge la Kaunti ya Taita Taveta lina jukumu muhimu la kutekeleza katika masuala ya utoaji wa huduma za afya kwa wakaazi wa kaunti hii. Hili li kwa mujibu wa Kifungu cha 185 moja(1) na mbili(2)cha Katiba ya Kenya, kuhusu utungaji wa sheria na kifungu cha 185 tatu (3) kinacholipa Bunge hili jukumu la usimamizi na uangalizi wa shughuli za Serikali ya Kaunti. Aya ya Pili ya Kiambatisho cha nne cha Katiba ya Kenya pia kinaeleza kuwa huduma za afya katika Kaunti ziko chini ya usimamzi wa Serikali za Kaunti.

Bunge hili linafahamu kuwa kila Mwananchi wa Taifa la Kenya ana haki ya kupata huduma bora za afya, kwa mujibu wa Katiba ya Kenya, kifungu cha 43 moja(1) na mbili(2). Kutokuwepo kwa wahudumu wa afya katika hospitali zetu kwa sababu ya mgomo wao, kunayaweka hatarani maisha ya wananchi wetu. Suala hili linaathiri pakubwa wananchi wanaoishi katika umaskini, ambao hawawezi kutafuta matibabu mbadala katika hospitali za kibinafsi, hivyo basi kuongeza pengo katika upokeaji wa huduma za afya.

Ingawaje Bunge Hili la Gatuzi la Taita Taveta halikupewa notisi hiyo ya mgomo iliyotumwa kwa afisi zingine ikiwemo Wizara ya Afya katika Kaunti hii, tunatambua umuhimu wa Bunge hili kwenye suala la huduma za afya. Kutokana na hilo, Bunge hili lilitoa mwaliko kwa idara mbalimbali za Kaunti hii kuja hapa Bungeni kuzungumzia swala hili la mgomo wa wahudumu wa afya na kuliweka wazi. Madhumuni ya mkutano huu ulikuwa kujaribu kusuluhisha masuala yanayotajwa kusababisha mgomo wa wahudumu wa afya, ili wananchi wa Kaunti hii waendelee kupata haki yao ya kupata huduma za afya. Hili lilifanywa Kulingana na Kifungu cha 195 cha Katiba ya Kenya, kinacholipa Bunge hili mamlaka ya kuwaalika watu kuja mbele ya Bunge, kwa ajili ya kutoa habari kwa Bunge hili.

Bunge hili, kupitia kwa Uongozi wake na Kamati ya Afya Bungeni, lilialika idara na maafisa mbalimbali katika Serikali ya Kaunti, ikiwa ni pamoja na Waziri wa Afya, Waziri wa Fedha,

Katibu wa Kaunti na Bodi ya Kuwaajiri Wafanyikazi ya Kaunti ya Taita Taveta. Mkutano huo umefanyika leo hii alasiri kulijadili suala la mgomo huu wa wahudumu wa afya.

Vilevile, Bunge hili kwa busara yake, liliwaalika wawakilishi wa Vyama vya wahudumu wa afya kuja mbele ya Bunge hili leo, asubuhi ya leo, kuyajadili malalamishi yao. Inasikitisha kuwa vyama vya wahudumu wa afya katika kaunti hii vimepuuza mwaliko huo na kususia mkutano na Bunge hili. Bunge hili lilikuwa na makusudi ya kutaka kuelewa kwa undani zaidi matatizo yanayowakumba, na kujaribu kutafuta njia mwafaka za kukomesha mgomo wao ambao umewaathiri wakaazi wengi wa Kaunti ya Taita Taveta.

Mkutano wa leo ulinuiwa kuendeleza mazungumzo yaliyoanza mnamo Tarehe 1 (moja) Mwezi wa Agosti, mwaka huu (2024) kati ya vyama mbalimbali vya kutetea haki za wafanyakazi hao wa afya na Bunge hili, ambapo hali ya huduma za afya katika Kaunti hii ilizungumziwa.

Bunge hili linatambua uzito wa masuala yanayowakumba Wahudumu wa Afya na kuwapelekea wao kugoma. Bunge hili pia lina madhumuni ya kuingilia kati kuona kwamba mikakati inawekwa na Serikali ya Kaunti kuyatatua matatizo hayo. Hata hivyo hilo haliwezekani ikiwa wahudumu wa afya wataendelea kukataa kuzungumza na Bunge hili, kama ilivyoshuhudiwa hapo awali leo.

Tunachukua fursa hii kuwaalika wahudumu wa afya kupitia kwa Wawakilishi wao na Vyama vya kupigania haki zao, kukubali kufanya mazungumzo na Bunge hili kwa ajili ya kusitisha mgomo wao na kurejesha huduma za afya katika kaunti yetu. Tunawasihi wahudumu hao wa afya Kuzingatia Kiapo walichokula kwamba maisha ya wagonjwa hayatakatizwa kwa kukosa huduma za afya.

Kwa kumalizia, Bunge hili linawasihi wahudumu wa afya wanaogoma kurejea kazini bila kusita, wakati ambapo mazungumzo yanaendelea na hatua zingine kuchukuliwa kushughulikia matatizo yanayowakumba na masuala mengine yanayowahusu. Bunge hili litahakikisha kuwa wahudumu wa afya wamesikilizwa na kutafuta njia mwafaka zaidi, kuona kuwa migomo hii ya mara kwa mara haitafanyika tena na kuendelea kuwaumiza wananchi wetu. Ila kwa sasa, tunawaomba warejee kazini, kuyaokoa maisha ya wananchi.

MHE. ANSELM MWADIME CHAO,

KAIMU SPIKA WA BUNGE LA KAUNTI

PO BOX 1142- 80304, WUNDANYI
Tel: 0718703359/0732604811
Facebook: Taita Taveta County Assembly
X: @ttcassembly
www.taitatavetaassembly.go.ke